JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI

04 **HISABATI**

Muda: Saa 2:00 **Mwaka : 2022**

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali **arobaini na tano (45)**.
2. Jibu maswali **yote**.
3. Soma maelekezo yote yaliyoko katika **fomu maalum ya kujibia (OMR)**.
4. Jaza taarifa zote katika fomu ya OMR.
5. Weka **kivuli** katika kila tarakimu ya **Namba yako ya Mtihani** kwenye nafasi husika katika fomu ya OMR.
6. Weka **kivuli** katika herufi ya jibu lililo sahihi kwa swali la **1** hadi **40** katika fomu yako ya kujibia uliyopewa. Kwa mfano, kama jibu sahihi ni A weka kivuli kama ifuatavyo:

~~[A]~~	[B]	[C]	[D]	[E]

7. Ukigundua kuwa herufi uliyowekea kivuli **si jibu sahihi**, futa kivuli hicho kwa umakini kwa kutumia **kifutio safi** kabla ya kuweka kivuli katika herufi mpya.
8. Tumia **penseli ya HB** tu katika kujibu swali la **1** hadi **40**, na kalamu ya wino wa **bluu** au **mweusi** kwa swali la **41** hadi **45**.
9. Onesha wazi njia iliyotumika katika kujibu swali la 41 hadi 45 katika nafasi iliyotolewa kwenye fomu ya OMR.
10. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.

2 207004 100011

CamScanner

SEHEMU A: MATENDO YA KIHISABATI, MAUMBO NA MAFUMBO

Katika swali la 1 – 40, kokotoa swali ulilopewa na kisha **weka kivuli** kwenye **herufi ya jibu lililo sahihi** katika fomu yako maalum ya kujibia (OMR) uliyopewa.

<table>
<tr><th>Na.</th><th>Swali</th><th>Sehemu ya Kazi</th></tr>
<tr><td>1.</td><td>Thamani ya nafasi ya tarakimu iliyopigiwa mstari katika namba 504251 ni
A Makumi
B Maelfu
C Mamia elfu
D Mamia
E Makumi elfu.</td><td>504251</td></tr>
<tr><td>2.</td><td>Jedwali lifuatalo linaonesha mauzo ya lita za petroli katika siku tano za wiki. Je, ni siku ipi lita nyingi zaidi za mafuta ziliuzwa?
<table>
<tr><th>Siku</th><td>Jumatatu</td><td>Jumanne</td><td>Jumatano</td><td>Alhamisi</td><td>Ijumaa</td></tr>
<tr><th>Lita</th><td>XLII</td><td>LXIX</td><td>XLIX</td><td>LXIV</td><td>XLIX</td></tr>
</table>
A Jumatatu
B Jumanne
C Jumatano
D Alhamisi
E Ijumaa</td><td></td></tr>
<tr><td>3.</td><td>Ipi kati ya sehemu $\frac{13}{14}$, $\frac{15}{14}$, $\frac{12}{13}$, $\frac{16}{17}$ na $\frac{19}{20}$ ni sehemu guni?
A $\frac{13}{14}$ B $\frac{15}{14}$ C $\frac{12}{13}$
D $\frac{16}{17}$ E $\frac{19}{20}$</td><td></td></tr>
</table>

CamScanner

Na.	Swali	Sehemu ya Kazi
4.	Ufaulu wa mwanafunzi wa Darasa la Saba katika masomo matano ulikuwa kama ifuatavyo: somo la Hisabati alipata $\frac{14}{25}$, Kiswahili alipata $\frac{5}{8}$, English Language alipata $\frac{1}{2}$, Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi alipata $\frac{3}{5}$ na Uraia na Maadili alipata $\frac{31}{50}$. Ni somo lipi alipata alama ndogo kuliko zote? A Hisabati B Kiswahili C English Language D Maarifa ya Jamii na Stadi za kazi E Uraia na Maadili	
5.	Mtungi wa gesi una ujazo wa lita 10. Iwapo lita 1.5 zimetumika, ni sehemu gani ya ujazo imebakia? A $\frac{17}{2}$ B $\frac{21}{20}$ C $\frac{17}{20}$ D $\frac{3}{2}$ E $\frac{3}{20}$	
6.	Upendo alimpa 0.1 ya kilogramu za sukari dada yake na $\frac{1}{5}$ shangazi yake. Ikiwa alibakiwa na kilogram 35, zipi kati ya zifuatazo ni jumla ya kilogramu za sukari alizokuwa nazo awali? A kg 500 B kg 50 C kg 35.3 D kg 38 E kg 45	
7.	Shule ya Msingi Mwenge ina jumla ya wanafunzi 560, ambapo kati yao $\frac{5}{8}$ ni wanachama wa skauti. Ikiwa $\frac{3}{5}$ ya wanachama wa skauti walilipa ada ya shule, ni asilimia ngapi ya wanafunzi hawakulipa ada? A 60% B 25% C 37.5% D 62.5% E 40%	

CamScanner

Na.	Swali	Schemu ya Kazi
8.	Mpeli alipewa kazi ya kupanga namba nzima zote zilizopo kati ya 22 na 55 ambazo ni vigawe vya 9. Upi ni mpangilio sahihi wa namba hizo ikiwa alianza na namba ndogo? A 27, 35, 49, 54 B 27, 42, 51, 54 C 27, 45, 51, 54 D 27, 36, 45, 54 E 27, 32, 45, 54	
9.	Mkulima alipanda michungwa kwenye mistari sita kwa mpangilio ufuatao: 90, 81, 72, _____, _____, 45. Michungwa iliyopandwa kwenye mstari wa nne na wa tano haikuota. Je, ni idadi ipi inawakilisha jumla ya michungwa ambayo haikuota? A 141 B 147 C 93 D 87 E 117	9 63 64 117
10.	Maria alimwomba kaka yake amsaidie kupanga namba XC, IV, LV, CI na VI kuanzia kubwa kwenda ndogo. Upi ni mpangilio sahihi? A CI, XC, LV, VI, IV B XC, CI, LV, IV, VI C CI, XC, VI, IV, LV D XC, LV,CI, IV, VI E CI, XC, LV, IV, VI	
11.	Wanafunzi watano walipewa kazi ya kuorodhesha vigawe vya 6 vilivyopo kati ya 30 na 60. Je, ipi ni orodha sahihi? A 36, 48, 54, 56 B 36, 48, 54, 60 C 36, 42, 54, 60 D 36, 42, 48, 54 E 36, 40, 42, 48	
12.	Wanafunzi watano waliorodhesha vigawe vitatu vya shirika vya namba 4 na 6 vilivyopo kati ya 10 na 40. Ipi ni sahihi kati ya orodha zifuatazo? A 16, 24, 36 B 12, 24, 36 C 12, 18, 36 D 16, 28, 36 E 12, 30, 36	

CamScanner

Na.	Swali	Sehemu ya Kazi
13.	Dotto ana jumla ya sh 1,200,000. Iwapo $\frac{2}{3}$ ya fedha za Dotto ni sawa na $\frac{1}{2}$ ya fedha za Kulwa, je, kati yao wawili mwenye kiasi kikubwa cha fedha kuliko mwenzake ana shilingi ngapi? A sh 800,000 B sh 600,000 C sh 400,000 D sh 1,600,000 E sh 1,200,000	
14.	Katika mojawapo ya hifadhi za Taifa kuna jumla ya wanyama 2,400,000. Ikiwa 0.3 ya wanyama wote ni Simba, 0.4 ni Swala, 0.2 ni Twiga na 0.1 ni Tembo, je, kuna tofauti ya wanyama wangapi kati ya kundi lenye wanyama wengi na kundi lenye wanyama wachache? A 720,000 B 240,000 C 1,200,000 D 480,000 E 960,000	0.4 0.3 0.2 0.1 1.0 10 2400000 10 2400000
15.	Zuhura ana uzito wa kilogramu 70.5 na Hamis ana uzito wa kilogramu 68.15. Je, jumla ya uzito wao ni kiasi gani? A 2.35 kg B 148.65 kg C 138.65 kg D 1.35 kg E 138.2 kg	70.5 68.15 138.65
16.	Jafari alipewa machungwa 789,951 na mlezi wake. Pia, alipata machungwa mengine 226,783 kutoka kwa rafiki yake. Je, jafari alipata jumla ya machungwa mangapi? A 563,232 B 1,016,734 C 563,168 D 1,016,634 E 916,734	789 951 + 226 783 1,016,734
17.	Jumla ya magari 834,223 yaliingizwa nchini mwaka 2020 kutoka Japani na nchi nyingine. Ikiwa magari 436,756 yalitoka Japan, je, magari mangapi yalitoka nchi nyingine? A 1,270,979 B 1,260,979 C 397,467 D 4,085,757 E 402,533	834 223 436 756 397 467

CamScanner

Na.	Swali	Sehemu ya Kazi
18.	Shamba la ng'ombe wa maziwa huzalisha lita 254,567 za maziwa kwa siku. Ni kiasi gani cha maziwa kitazalishwa kwa siku 43? A Lita 10,947,381 B Lita 10,846,381 C Lita 254,524 D Lita 254,610 E Lita 10,946,381	254567 43 254610
19.	Tatu alikuwa na shilingi 5,500 alizopata katika biashara yake. Ikiwa alitumia $\frac{2}{5}$ ya fedha hizo kununua matunda alibakiwa na kiasi gani cha fedha? A sh 2,200 B sh 7,700 C sh 3,300 D sh 1,100 E sh 4,400	$\frac{5,500}{1} \times \frac{2}{5}$ 13600 2500 2 = 27500 5500 5 05002 12500 7500 11500
20.	Sharifa alikuwa na shilingi 47,200 kwenye akaunti yake. Ikiwa alinunua suruali 3 za watoto wake kwa bei ya shilingi 12,900 kila moja, je, alibakiwa na kiasi gani cha fedha? A sh 38,700 B sh 12,900 C sh 34,300 D sh 8,500 E sh 60,100	47200 12900 34400
21.	Amina alitumia $\frac{1}{3}$ ya mshahara wake wa mwezi kununua nguo na $\frac{1}{2}$ ya kiasi kilichobaki kununua chakula. Ikiwa alibaki na sh 400,000 baada ya matumizi hayo, je jumla ya mshahara wake kwa mwezi ni kiasi gani? A sh 2,000,000 B sh 1,600,000 C sh 1,200,000 D sh 2,400,000 E sh 2,800,000	
22.	Katika shule ya msingi Magomeni kuna wasichana 450 zaidi ya idadi ya wavulana. Ikiwa $\frac{3}{4}$ ya wanafunzi ni wasichana, kuna wanafunzi wangapi katika shule hiyo? A 900 B 225 C 1,125 D 675 E 800	$\frac{450}{1} \times \frac{3}{4}$ 450 × 4 = 3 × 1 600 $\frac{1800}{3} = \frac{3}{3}$

CamScanner

Na.	Swali	Sehemu ya Kazi
23.	Zaina alitumia shilingi 4,800 kutuma maneno 63 kwa simu ya maandishi. Ikiwa maneno 30 yalitozwa shilingi 50 kwa kila neno; je, maneno 33 yaliyobaki yalitozwa jumla ya shillingi ngapi? A Shilingi 3,300 B Shilingi 100 C Shilingi 1,500 D Shilingi 1,650 E Shilingi 110	
24.	Zahara alikuwa na sh 326,550. Iwapo alitumia sh 211,400, alibakiwa na kiasi gani? A sh 115,150 B sh 537,950 C sh 537,150 D sh 538,050 E sh 115,950	326550 211400 537950
25.	Kuna miaka na miezi mingapi katika miezi 92? A Miaka 8 miezi 0 B Miaka 9 miezi 2 C Miaka 7 miezi 2 D Miaka 9 miezi 8 E Miaka 7 miezi 8	
26.	Jamali hutumia muda wa siku 50 kuandaa bustani ya mboga. Je, muda huo huandikwaje kwa mtindo wa wiki na siku? A Wiki 7 na siku 1 B Wiki 4 na siku 2 C Wiki 8 na siku 2 D Wiki 7 na siku 0 E Wiki 1 na siku 20	
27.	Ipi ni jumla ya fedha zifuatazo: sh 5,707 na st 35, sh 2,983 na st 80 na sh 1,245 na st 40? A sh 9,935 na st 55 B sh 9,935 na st 45 C sh 9,935 na st 65 D sh 9,936 na st 15 E sh 9,936 na st 55	35 40 80 155
28.	Mwajuma aliweka kiasi cha shilingi 564,000 katika benki inayotoa kiasi cha riba ya $5\frac{1}{2}$% kwa mwaka. Je, alipata riba ya kiasi gani kwa miezi 6? A Shilingi 31,020 B Shilingi 18,612 C Shilingi 60,040 D Shilingi 15,510 E Shilingi 186,120	

CamScanner

Na.	Swali	Sehemu ya Kazi
29.	Mchoro ufuatao ni sanduku la nguo lenye umbo la mchemstatili ambao umefungwa pande zote.  Je, eneo lililotiwa kivuli ni sehemu gani ya eneo la umbo zima? A $\frac{1}{10}$ B $\frac{1}{7}$ C $\frac{1}{6}$ D $\frac{2}{7}$ E $\frac{5}{21}$	
30.	Lita ngapi za maziwa zinahitajika kujaza chombo chenye umbo la mchemraba ufuatao ikiwa lita 1 =sm^3 1,000?  A 8.0 B 80 C 800 D 0.8 E 2.4	
31.	Juma alilima meta 200 za mraba za shamba lake lenye urefu wa meta 20 na upana wa meta 14. Je, meta ngapi za mraba hazikulimwa katika shamba hilo? A m^2 166 B m^2 234 C m^2 80 D m^2 280 E m^2 480	

CamScanner

Na.	Swali	Sehemu ya Kazi
32.	Mchoro ufuatao unaonesha kitalu cha nyanya chenye umbo la pembetatu pacha. Ikiwa mzingo wa kitalu chote ni sm 64, tafuta eneo lake.  A sm^2 100 B $sm^2$192 C sm^2 56 D $sm^2$320 E sm^2 384	
33.	Chupa ya maji ina ujazo wa ml 350. Je, katoni 2 za chupa za maji zina jumla ya lita ngapi ikiwa kila katoni ina chupa 24? A lita 1.68 B lita 168 C lita 1,680 D lita 16.8 E lita 0.168	
34.	Mzedema aliwapa watoto watano maziwa lita 8.06, lita 80.6, lita 0.86, lita 8.6 na lita 0.806 na kuwapanga katika mstari kulingana na ujazo wa maziwa waliyopewa, kuanzia ujazo mdogo hadi mkubwa. Je, ni kiasi gani cha maziwa alipewa mtoto aliyekuwa nafasi ya tatu katika mstari huo? A lita 8.06 B lita 80.6 C lita 0.86 D lita 8.6 E lita 0.806	
35.	Damasi ana kamba yenye urefu wa km 6 sm 1. Ikiwa urefu wa kamba ya Roni ni pungufu ya urefu wa kamba ya Damasi kwa km 2 m 8 sm 4, tafufa urefu wa kamba ya Roni. A km 3 m 1 sm 7 B km 3 m 1 sm 97 C km 3 m 91 sm 97 D km 3 m 991 sm 7 E km 3 m 991 sm 97	
36.	Nahodha alisafiri kwa mwendokasi wa km 24 kwa saa. Ni umbali gani alisafiri kwa muda wa saa 2 na dakika 30? A km 60 B km 3,600 C km 720 D km 768 E km 48	

CamScanner

Na.	Swali	Sehemu ya Kazi
37.	Herufi y katika mlinganyo $\frac{2}{y}+\frac{3}{y}=\frac{5}{8}$ inawakilisha namba ipi? A 5 B 8 C 1 D 3 E 2	
38.	Iwapo $2n^2 - 128 = 0$, tafuta thamani ya n. A 64 B 8 C 32 D -64 E -32	
39.	Wastani wa vimo vya wanafunzi tisa wa Darasa la Saba ni sentimeta 150. Ikiwa jumla ya vimo vya wanafunzi 4 ni sentimeta 450, wastani wa vimo vya wanafunzi watano waliobaki utakuwa sentimeta ngapi? A 1,350 B 900 C 4,500 D 180 E 300	
40.	Jedwali lifuatalo linaonesha idadi ya wagonjwa wa malaria waliolazwa katika kituo cha afya cha Kariko kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo: **Mwaka** | **Idadi ya Wagonjwa** 2016 | 208 2017 | 150 2018 | 237 2019 | 173 2020 | 127 Je, upi wastani wa wagonjwa waliolazwa kwa mwaka? A 179 B 192 C 768 D 895 E 237	

CamScanner

SEHEMU B: MATENDO YA KIHISABATI, MAUMBO NA MAFUMBO

Katika swali la 41 – 45, onesha wazi njia iliyotumika kutafuta jibu kwa kutumia **kalamu ya wino wa bluu** au **mweusi** katika nafasi iliyotengwa kwenye fomu ya OMR.

41. Bwana Nguvumali alinunua mbegu za mahindi kwa sh 1,600. Ikiwa bei ya kilogramu 1.75 za mbegu za mahindi sokoni ni sh 11,200, je, alipata kiasi gani cha mbegu za mahindi?

42. Bustani ya shule yenye umbo la mstatili ina eneo la m^2 9,632. Iwapo urefu wa bustani hiyo ni meta 112, je, mzingo wa bustani nzima utakuwa meta ngapi katika mamia yaliyo karibu?

43. Bahati alitembea umbali wa meta 400 kutoka nyumbani kwenda shuleni na kisha alitembea umbali wa meta 300 kutoka shuleni kwenda hospitali kama inavyoonekana katika mchoro ufuatao.



Je, alitembea umbali gani kutoka hospitali kwenda nyumbani kwa kupita njia fupi?

44. Bibi hutumia muda wa saa 3 kupika chakula. Iwapo alianza kupika saa 03:45, je, alimaliza kupika saa ngapi katika mfumo wa saa 12?

45. Kapiligali alikuwa na mtaji wa sh 85,000. Alinunua vikapu 13 @ sh 250, chumvi dazeni 3 @ sh 1,200, mafuta ya kupikia kwa sh 4,500, nyanya kg 3 @ sh 1,300 na mchele kg 5 @ sh 2,000. Je, Kapiligali alibakiwa na shilingi ngapi?

CamScanner